NyumbayaMaarifa (NIP) Opposite ATCL House, 1st Floor, Ohio Street,
P.O. Box.79868, Dar es Salaam. Tel: +255 22 2127464, Fax: +255 22 2126399,
Email: tapsea2014@gmail.com Website: http://www.tapsea.or.tz

**Kumb. Na.:** TAPSEA/2021/B/8/M/63 **Tarehe:** ………………………..

…………………………………………….
…………………………………………….
…………………………………………….
**……………………………………**

YAH: **MKUTANO WA KITAALUMA NA MKUTANO MKUU WA MAKATIBU MAHSUSI TANZANIA UTAKAOFANYIKA KUANZIA TAREHE 20 HADI 22 MEI, 2021 KATIKA MKOA WA ARUSHA**

Kichwa cha barua hapo juu cha husika.

Chama cha Makatibu Mahsusi Tanzania (TAPSEA), kina utaratibu wa kufanya Mkutano Mkuu na Mkutano wa Kitaaluma mara moja kila mwaka. Kwa mantiki hiyo, mwaka huu wa 2021 Mkutano huo utafanyika tarehe 20 hadi 22 Mei, 2021 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa (AICC) Arusha.

Kwa kawaida Mkutano hutanguliwa na mada mbalimbali ambazo zitawasilishwa na Wakufunzi mahiri wenye fani mbalimbali za Utumishi wa Umma zenye lengo la kuelimisha Wasaidizi wa Watendaji Wakuu, Waandishi Waendesha Ofisi, Makatibu Mahsusi Waandamizi na Makatibu Mahsusi wote pamoja na kukumbushana, kubadilishana mawazo, maarifa na uzoefu wa kiutendaji ili kuimairisha uboreshaji na utendaji kazi kwa maslahi ya Taifa. Baada ya Mafunzo hayo washiriki wote wanapatiwa vyeti vya ushiriki.

Kauli Mbiu ya Mkutano wa mwaka 2021 ni; **Kuwa Mbunifu Mahiri, Zingatia Weledi katika kuleta Mabadiliko ya Uchumi Tanzania ("*Be a Creative Professional, focus on improvising in advancing economic transformation in Tanzania").*** Aidha, Makatibu Mahsusi kutoka taasisi mbalimbali za serikali na Umma hutoa mchango mkubwa katika mafanikio ya Chama cha Makatibu Mahsusi Tanzania.

Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa **Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa (MB) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora** Kwa barua hii tunaomba uwaruhusu Makatibu Mahsusi na kuwalipia gharama zote za kushiriki katika Mkutano huuwa Kitaaluma wa mwaka 2021.

**Kwa nini Kushiriki Mkutano wa Kitaaluma kwa Mwaka 2021:**

Makatibu Mahsusi wanauhitaji mkubwa wa kupata ujuzi mpya na maarifa mapyalli kukabiliana na changamoto ambapo wanahitajika wawe na uwanja mpana wa kupata ufumbuzi wachangamoto wanazo kutana nazo, kwa sababu hiyo:

- Mkutano huu wa Kitaaluma utawasaidia kuibua njia mbalimbali za kupita ili kufikia kiwango cha juu kwenye kada yao na kuwaongezea thamani;
- Kupata uzoefu, weledi na umahiri kwa kufanyakazi kwa ushirikiano ili kufikia malengo husika;
- Kuleta ongezeko la thamani kwa taasisi ili taasisi ifanyekazi kwa weledi;
- Kumuongezea Katibu Mahsusi ujasiri katika majukumu yakeya kila siku;
- Kujenga uwezo wa kumudu kazi za kila siku.

**MTAZAMO:** Ni wajibu wakila Katibu Mahsusi kuonyesha umahiri katika Nyanja ya Utawala na anatarajiwa kuwa na kiwango cha juu katika mawasiliano ya kikazi.

**UJUZI:** Katibu Mahsusi anatakiwa kuwa na ujuzi kwenye Nyanja mbalimbali ili afanyekazi kwa weledi kukidhi mahitaji ya Kitaifa na Kimataifa ya sayansi na tekinolojia.

**USHIRIKIANO:** Katibu Mahsusi ni kiungo muhimu kwa taasisi kwa kuhakikisha waajiriwa wote wanafanyakazi kwa ushirikiano

**GHARAMA ZA USHIRIKI:**

Gharama za ushiriki wa Mkutano Mkuu wa Kitaaluma kwa mwaka 2021 ni **Shilingi 400,000/=;** Kwa wanachama ambao mwaka 2020 hawakulipa ada ya mwaka ya Tshs **50,000/=** watatakiwa kulipia **450,000/=** za Kitanzania. Tunaomba fedha hizi zilipwe na mwajiri moja kwa moja kwenye akaunti za Benki badala ya kupewa washiriki mkononi ili kuzuia ucheleweshwaji wa malipo kwa wakati. Malipo ya fedha taslimu hayatapokelewa Ofisi za Chama (TAPSEA). Tafadhali unaombwa kulipia ada ya ushiriki mapema ili kukamilisha maandalizi. Mwajiri anatakiwa amlipie Mshiriki fedha ya kujikimu kulingana na taratibu za ofisi au Taasisi husika.

Malipo yote yafanyike kwenye akaunti za Benki zifuatazo: -

1. Jina la Akaunti: **"Tanzania Personal Secretaries Association"**
   Benki: NMB, Tawi la NMB House,
   Akaunti No: **22306600363**

2. Jina la Akaunti: "**Tanzania Personal Secretaries Association"**
   Benki: CRDB Bank Plc, Tawi la Azikiwe,
   Akaunti No: **0150031411800**



***Tuendelee kuchukua tahadhari ya kujikinga na Corona kwa kunawa mikono na sabuni kwa maji tiririka, kuvaa Barakoa, kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu na kutumia kitakasa mikono (sanitizer)***

**Muhimu:**

**(i)** Washiriki wote walioko Dar es Salaam, baada ya kufanya malipo, wawasilishe stakabadhi ya malipo ya Benki katika Ofisi za TAPSEA zilizopo mtaa wa Ohio Nyumba ya Maarifa Mkabala na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ili waweze kupatiwa risiti. Kwa wale washiriki wa Mikoani na Zanzibar, ukishalipa tuma hati ya malipo kwa barua pepe ifuatayo **tapsea2014@gmail.com** pamoja na orodha ya majina ya washiriki.

Hakikisha kwenye Stakabadhi ya malipo unaandika jina lako kamili, Taasisi unayotoka namba ya simu kwa mawasiliano na kumbukumbu. Tafadhali lipa malipo ya kushiriki Mkutano kabla ya tarehe 15 Mei, 2021 na kujisajili mapema ili kuondoa usumbufu. Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu zifuatazo; +255754496027/+255754492114/ +255717648155.

(ii) **Vazi Rasmi**: **Kitenge au Suti;** Kitenge au **Suti zenye muonekano waheshima.**

Asante sana kwa ushirikiano wako.

Wako katika ujenzi wa Taifa,
**CHAMA CHA MAKATIBU MAHSUSI TANZANIA (TAPSEA)**

TANZANIA PERSONAL SECRETARY
ASSOCIATION (TAPSEA)
P. O. Box 79868
DAR ES SALAAM

Bibi Aneth Charles Mapima
**KATIBU MKUU**



***Tuendelee kuchukua tahadhari ya kujikinga na Corona kwa kunawa mikono na sabuni kwa maji tiririka, kuvaa Barakoa, kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu na kutumia kitakasa mikono (sanitizer)***

## PARTICIPATION FORM

From: Tanzania Personal Secretaries Association,
P. O. Box 79868
**DAR ES SALAAM**

| **Name of Organization:** ………………………………………………………………………………… | | **Mobile Number** |
|---|---|---|
| **S/No.** | **Name (s) of Participant (s)** | |
| **1.** | | |
| **2.** | | |
| **3.** | | |
| **4.** | | |
| **5.** | | |
| **6.** | | |
| **7.** | | |
| **8.** | | |
| **9.** | | |
| **10.** | | |
| **11.** | | |
| **12.** | | |
| **13.** | | |
| **14.** | | |
| **15.** | | |

I/We accept to attend
……………………………………………………………………

TANZANIA PERSONAL SECRETARY
ASSOCIATION (TAPSEA)
P. O. Box 79868
DAR ES SALAAM

**FOR REGISTRATION:**

For payments by cheque or cash deposit please send a scanned copy of your payment slip to tapsea2014@gmail.com or Fax 225 22 2126399.

I/We enclose herewith **Cheque or Pay in Slip of Tshs**……………………………. being our participation costs for TAPSEA Annual Conference and 8th General Meeting 2021.



*Tuendelee kuchukua tahadhari ya kujikinga na Corona kwa kunawa mikono na sabuni kwa maji tiririka, kuvaa Barakoa, kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu na kutumia kitakasa mikono (sanitizer)*